# Misingi ya Ukalimani na Tafsiri

## Kwa Shule, Vyuo na Ndaki





SERENGETI BOOKSHOP

Fred Simiyu Wanjala

# Misingi ya Ukalimani na Tafsiri

## Kwa Shule, Vyuo na Ndaki




*Fred Simiyu Wanjala*

**KIMECHAPISHWA NA:**

**SERENGETI BOOKSHOP**
P.O. BOX 11132
MAKOROBOI STREET
MWANZA, TANZANIA
MOBILE: + 255 784 281 942
FAX: +25528254215
Email: serengetibookshop@yahoo.com.

**© Serengeti Bookshop**
**© Wanjala F. Simiyu 2011**

**MWANDISHI:**
Fred Simiyu Wanjala

**MHARIRI MSANIFU:**
*Ndesika J. Msaki*
*E-mail: ndesika2002@yahoo.com*

**ISBN: 9987 - 478 -**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa njia yoyote ile bila idhini ya **SERENGETI BOOKSHOP.**

## Dibaji

Misingi ya Ukalimani na Tafsiri ni tunu adimu kwa watu wote wenye ari ya kutafuta maarifa na hekima. Utafiti na uandishi juu ya tafsiri umepiga hatua kubwa baada ya kufunguliwa rasmi na kina Catford, Holmes, Larson, Newmark, Nida na Jean, ila vitabu vyao vimeandikwa kwa Kiingereza. Baada ya jamvi la tafsiri kufunguliwa, mtaalam Prof. Mwansoko aliokoa umma wa Kiswahili kwa kuchapisha kitabu cha kwanza cha tafsiri kwa Kiswahili; Kitangulizi cha Tafsiri;

Nadharia na Mbinu. Mwalimu Mshindo naye ametoa mchango wake kwa kuandika kitabu cha pili cha tafsiri kwa Kiswahili; Tafasiri na Kufasiri. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa taaluma hii ya tafsiri, bado kuna mengi mbele ya safari. Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kinatazamiwa kushadidia juhudi hizi kwa kutilia makazo eneo ambalo linaelekea kuwa bikra; Ukalimani. Kitabu hiki kimekamilika baada ya utafiti wa takriban miaka minane.

Safari ya kuandika Misingi ya Ukalimani na Tafsiri ilichochewa na mihangaiko niliyopata wakati nasomea shahada yangu ya kwanza, katika Ndaki ya Kenyatta na baadaye wakati wa kuifundisha kozi ya tafsiri katika Ndaki mbalimbali. Changamoto hizi zilitokana na kuwepo kwa kitabu kimoja tu cha tafsiri, cha baba wa tafsiri, Prof. Mwansoko. Kitangulizi cha tafsiri; Nadharia na mbinu, kilikuwa kama dhahabu kwani kulikuwa na nakala tano tu katika maktaba ya Ndaki ya Kenyatta.

Wanazuoni walilazimika kukisoma kwa zamu, kwa vilemba na kwa kukitunza katika sehemu maalum maktabani, ili wengine wasikipate! Mambo yalikuwa magumu zaidi, nilipoanza kufundisha, kwani iliniwia vigumu kutumia marejeleo ya kitabu kimoja tu katika kozi ya tafsiri. Matatizo haya ndiyo yalikuwa chachu ya kuanza safari ndefu ya kuandika Misingi ya Ukalimani na Tafsiri. Matokeo ya safari yangu iliyoanzia chuoni yamesadifu methali: mwanzo wa ngoma ni lele. Ni matumaini yangu kuwa, Misingi ya Ukalimani na Tafsiri, kitakuwa na msaada mkubwa kwa wanafunzi, walimu na wahadhiri wa somo la ukalimani na tafsiri.

Nisingefaulu bila msaada wa watu mbalimbali. Nitakuwa mkosa fadhila iwapo sitawapa mkono wote waliochangia katika kuiumba kazi hii, ama moja kwa moja ua kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mosi, ningependa kumtolea Mola shukrani zisizo kipimo kwa kunikirimia neema na baraka zake katika maisha yangu. Pili, napenda kumshukuru mke wangu mpendwa, Annette kwa maoni na mapenzi yake yaliyochangia pakubwa katika kukikamilisha kitabu hiki.

Aidha, nawashukuru wazazi wangu wapendwa: Marehemu babangu Francis Nyongesa Wanjala (Mungu aiweka roho yake pema peponi) na mamangu Margaret Lusike Buyabo kwa malezi yao mema na azma yao ya kutaka kuelimisha watoto wao. Vile vile, nampongeza ndugu yangu Daniel Wafula Wanjala kwa msaada wake wa hali na mali.

Tatu, nawapa tahania wataalam na wasanii mbalimbali ambao nimezinukuu kazi zao. Nawaomba wote wachukulie kuwa kuwanukuu kwangu ni ishara tosha ya kuwapongeza na kuzivulia kofia kazi zao jamali.

Nne, nawavulia kofia walimu wangu; Hayati Mathias Murambi, Marehemu mama Asmin Osemo Wekesa, James Makokha, Julius Wafula, Dennis Wekesa, Robert Masese, Dkt. Miriam Osore, Prof. Kitula King'ei, Prof. Ireri Mbaabu, Dkt. Jackton Onyango, Dkt. Leonard Chacha, Dkt. Petronilla Mathooko, Dkt. Alice Mwihaki, Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Richard Wafula kwa msaada wao mkubwa wa kitaaluma ulioniandaa vyema nikawa nilivyo sasa. Kwa namna ya pekee, namhongera Dkt. Miriam Osore kwa kunifundisha kozi za Ukalimani na Tafsiri nilipokuwa nahangaikia shahada yangu ya kwanza, katika Ndaki ya Kenyatta. Aidha, namshukuru sana Prof. Senkoro kwa ushauri wake mzuri wa kitaaluma na kwa kukubali kukiandikia utangulizi;Misingi ya Ukalimani na Tafsiri.

Tano, napenda kuwapongeza wahadhiri wenzangu; Samwel Riro, Mary Malenya, James Wanyela, Jackson Kavoi, Crispin Isaboke na Kolins Ocham kwa kunipa maoni na moyo wa kuniwezesha kukamilisha Misingi ya Ukalimani na Tafsiri, baada ya kupitia muswada wangu. Sita, nampongeza Serengeti Bookshop kwa kukubali kukifadhili kitabu hiki. Pia namshukuru Msaki kwa kukisarifu kitabu hiki kwa kiwango jamali.

Mwisho, nawapa heko wanafunzi wangu walionisaidia kwa njia moja au nyingine kuhitimisha safari hii ngumu. Wanafunzi wangu walinitia moyo walipoyapokea maoni mbalimbali ya Misingi ya Ukalimani na Tafsiri, kikiwa katika hatua za mwanzo. Sitaweza kuwataja wote: baadhi ya wanafunzi wangu wapendwa ni pamoja na; Justine Bake, Stella Benedicto, Pamella, M. Felix, Fr. Urick Kinyero na Athumani Adam Hamisi. Wengine wote ambao sikuwataja, nasema asanteni sana na Mterehemezi awamiminie baraka chungu nzima. Nawashirikisha walioniauni wote katika ufanisi wa Misingi ya Ukalimani na Tafsiri. Hata hivyo, ninakubali kuubeba msalaba wa upungufu wowote utakaojitokeza katika Misingi ya Ukalimani na Tafsiri.

**Fred Simiyu Wanjala,**
**Ndaki ya Mtakatifu Agostino, Tanzania,**
**Septemba, 2011.**

Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kimeandikwa kwa ustadi na kwa makini ili kimfae msomi yeyote. Mwandishi ametoa ufafanuzi wa dhanaza ukalimani,ukafsiri, kufasilina tafsirikwa mapanayake. Aidha, maelezo ya kina kuhusu aina za ukalimani na tafsiri, taaluma zinazojenga tafsiri na ukalimani, mchakato wa kufasiri pamoja na uhakiki wa ukalimani na tafsiri yametolewa kwa undani. Vile vile, mwandishi ametoa mazoezi baada ya kila sura ili kumpa msomaji nafasi ya kujipima anapoendelea kusoma Misingi ya Ukalimani na Tafsiri. Kitabu hiki kinawafaa wanafunzi, wanazuoni, walimu na wahadhiri wa taaluma zote katika ngazi zote za elimu.



Fred Simiyu Wanjala, mwandishi wa Kitabu hiki ni msomi na mwalimu wa fasihi, lugha na isimu aliye na tajiriba pana ya ufundishaji. Ana shahada ya Uzamili (Kiswahili), kutoka Ndaki ya Kenyatta, (Kenyatta University). Amewahi kufundisha katika shule mbalimbali; Shule ya Upili ya Maliki (Bungoma), Shule ya Upili ya Mandera Integrated Academy (Mandera), Shule ya Wasichana ya Bulimbo (Mumias), Shule ya Thika Road Academy (Nairobi) na Shule ya Upili ya Kapkures (Bomet). Aidha, amefundisha katika Ndaki za Moi Bewa la Kabianga na Egerton Bewa la Kisii kama Mhadhiri wa muda. Kwa sasa, yeye ni mhadhiri wa Isimu, Lugha na Fasihi ya Kiswahili, pamoja na kozi ya Tafsiri katika Ndaki ya Mtakatifu Agostino, Tanzania. (St. Augustine University of Tanzania). Yeye ndiye mwandishi wa kitabu maarufu cha Kitovu cha Fasihi Simulizi.

ISBN:9987-478-

**Kimechapishwana:**

SERENGETI BOOKSHOP